

Maswali na Majibu

1. Mbona watawala wa Wayahudi walikasirika?
Kwa sababu wanafunzi walikuwa wakifundisha kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu tena alikuwa amefufuka kutoka kwa wafu.
2. Watawala wa Wayahudi walifanyaje Petro na mitume wengine?
Waliwatia gerezani.
3. Kuwafanya hivyo iliwazuia kuhubiri Injili?
Hapana. Malaika aliwatoa gerezani.
4. Watawala wa Wayahudi walifanyaje Stefano?
Waliwahonga watu kusema uongo juu yake na wakampiga kwa mawe mpaka akafa.
5. Hawa watawala waliendelea na kufanyaje Wakristo waliokuwa Yerusalemu?
Waliwatesa.
6. Haya yalizuia Injili kuhubiriwa?
Hapana. Wakristo walienda kwa miji mingine na kueneza Injili.
7. Filipo alielezea Mkushi nini?
Alimweleza juu ya Yesu na tumaini ya uzima wenye atapea wote wanaoamini.
8. Filipo na Mkushi walifanya nini walipofika kwa maji?
Filipo alibatiza yule Mkushi.
9. Kornelio alikuwa nani? Malaika alimwambia afanye nini?
Alikuwa askari na Mtaifa. Malaika alimwambia atumanishe Petro aje.
10. Peana sababu mbili zilizofanya Petro ambatize Kornelio hali alikuwa Mtaifa.
Mungu alikuwa amemwonyesha kwa ndoto kwamba hata watu wa Mtaifa wanaweza kuwa watu wa Mungu. Kornelio alipata Roho Mtakatifu.

Mistari ya kukariri

Matendo 4:19 – 20 Matendo 10:15 Matendo 10:47 Wagalatia 3:26 – 29

Mazungumzo

Soma Matendo 8:36 – 39. Zungumza juu ya somo lenye tunapata kwa hizi mistari.

Kuandika

Soma Matendo 10:9 – 20. Andika juu ya ndoto yenye Mungu alipea Petro. Hiyo ndoto ilifundisha Petro nini?

Masomo ya watoto wakubwa wa CBM



Somo la 40 Wanafunzi wanahubiri Injili

SOMA Matendo 5:17 – 42; 6:1 – 15; 7:54 – 60; 8:26 – 39; Matendo 10

SOMO

Watawala wa Wayahudi walikasirika sana walipoona watu wengi wanaamini kwa Yesu. Walikasirika kwa sababu wanafunzi walifundisha na kufanya miujiza katika jina la Yesu. Watawala wa Wayahudi walikuwa wameua Yesu. Walifikiri wamegomesha mafundisho yake. Walikasirika sana kwa sababu wanafunzi waliendelea kufundisha juu ya Yesu na watu wengi waliwaamini. Watawala wa Wayahudi walikasika zaidi walipokundua kwamba wanafunzi walikuwa wakifundisha kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu na eti amefufuka kutoka kwa wafu.

Watawala wa Wayahudi waliamrisha wanafunzi wasifundisha juu ya Yesu. Petro aliwambia kwamba ni la maana sana kutii Mungu kuliko kutii mwanadamu. Yesu Mwana wa Mungu, aliwaamrisha wao wafundishe kwa jina lake. Lazima wamtii. Watawala wa Wayahudi walishika Petro na mitume wengine na kuwaweka gerezani ili wagome kufundisha. Lakini malaika aliwatoa gerezani. Wanadamu hawawezi kuzuia kufundisha na kufanya kusudi ya Mungu.

Watu walioamini kwa Yesu na kubatizwa, baadaye waliitwa Wakristo. Wakristo waliokutana pamoja kuabudu Mungu waliitwa kanisa. Watawala wa Wayahudi walikasirika sana walipoona watu wengi wanaamini mafundisho ya wanafunzi na kuwa Wakristo. Wakati ule, kulikuwa na maelefu ya Wayahudi waliokubali kuwa Wakristo hapo Yerusamu.

Stefano alikuwa kijana Mkristo aliyefanyia kanisa kazi nyingi. Watawala wa Wayahudi walionga watu wabaya kusema uongo juu ya Stefano. Stefano alishikwa na kupelekwa kwa Baraza ya watawala. Wale watu wabaya walisema uongo juu ya Stefano na kuchochea watu kinyume nae. Watawala wa Wayahudi walikasirika sana na kumburura Stefano nje ya Yerusalemu, wakampiga kwa mawe mpaka akafa.

Baada ya kifo cha Stefano, watawala walitesa Wakristo wote waliokuwa Yerusalemu. Wakristo wengi walitoka Yerusalemu na kwenda kuishi kwa miji mingine. Lakini hawa watawala hawakuweza kuzuia Injili kuenezwa. Popote Wakristo walienda, walihubiri Injili. Kanisa ya Wakristo ilianza kwa kila mji wa nchi ya Israeli. Wanadamu hawawezi kuzuia mafundisho na kusudi ya Mungu.

Wanafunzi walihubiria Wayahudi wa Yerusalemu na nchi yote ya Israeli. Baadaye wanafunzi waliitwa 'mitume' maana yake 'mtu aliyetumwa.' Yesu alikuwa amewatuma wahubiri Injili. Filipo alihubiri Injili kwa vijiji vingi sana vya Samaria. Siku moja malaika akamwambia aende chini kuelekea jangwani. Kule aliona mtu aliyetoka kushi (Ethiopia) kwa gari akisoma Agano la Kale. Huyu mtu towashi alifanya kazi kwa nyumba ya malikia wa Kushi aitwaye Kandake. Alikuwa anatoka Yerusalemu kuabudu na anarudi nyumbani.

Huyo Mkushi alikuwa anasoma kitabu cha Isaya 53:3 – 7 lakini hakukuwa akielewa. Hakujua kama Isaya alisema juu ya yeye mwenyewe au juu ya mtu mwingine. Filipo alipanda juu ya gari la towashi na akamwelezea maana ya hizo mistari. Filipo alimwambia yote juu ya Yesu. Alimwelezea kwamba manabii wa Agano la Kale waliandika habari juu ya Yesu. Alimwambia juu ya tumaini kubwa ya uzima wenye Yesu atapea wote wanaomwamini.

Mkushi alielewa habari njema ya Yesu na akafurahi sana. Walipofika kwa maji, aliuliza Filipo ambatize. Filipo alimuuliza kama kweli anaamini na moyo wake wote angeweza kubatizwa. Towashi alitikia kwamba anaamini kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu. Filipo na towashi walitelemka mpaka kwa maji na Filipo akambatiza ndani ya maji. Halafu Filipo akamwacha Mkushi na akaendelea na safari yake akiwa amefurahi.

UBATIZO

Filipo aliakikisha kwamba Mkushi ameelewa na kuamini Injili ndiyo ambatize. Lazima tuelewe habari ya Yesu na ya Ufalme wa Mungu ndiyo tubatizwe.

Filipo na towashi walienda ndani ya maji pamoja. Walikuwa jangwani na labda huyu Mkushi alikuwa na maji ya kunywa kwa chupa. Lakini kunyunyishia mtu maji, sio ubatizo. Waliongoja mpaka walipofika kwa maji ya kutosha ya kumwingiza Mkushi ndani kabisa, ndio ubatizo.

Wakristo wa kwanza walikuwa Wayahudi. Ahadi za Mungu za wokovu katika Yesu zilipewa Abrahamu na Daudi. Wayahudi walipewa hizi ahadi za Mungu. Unakumbuka ahadi ya Mungu kwa mzao wa Ibrahimu (Yesu) italeta baraka kwa watu wa mataifa yote. Mungu alitaka Yesu kama dhabihu alete wokovu kwa watu wote.

Yesu alikuwa Myahudi. Watu wa mataifa wakibatizwa, wanakuwa wamoja kwa familia ya Mungu na kuwa ndugu au dada wa Yesu. Watu wamataifa ni Wayahudi wanaopandikizwa na wanaweza kushirikishwa kwa ahadi za Mungu. Wanasamehewa dhambi zao kupitia kwa Yesu. Wanaweza kuwa na tumaini la uzima kwa Ufalme wa Mungu.

Kornelio alikuwa askari aliyeishi Kaisaria. Kornelio alikuwa Mtaifa lakini alikuwa mtu wa imani. Aliomba Mungu kila wakati na alisaidia maskini. Siku moja alipokuwa akiomba, malaika alimkujia na kumwambia atume mtu aite Petro aje. Malaika aliambia Kornelio kwamba Petro atamwambia nini Mungu anataka afanye.

Baada ya siku ghadhaa Petro alifika kwa nyumba ya Kornelio. Petro alikuwa Myahudi na Kornelio alikuwa Mtaifa. Wayahudi ni watu wateule wa Mungu. Katika Agano la Kale, Mungu aliambia Wayahudi wajitenge na watu wa Mataifa. Wayahudi walifikiri watu wa Mataifa ni wanajisi. Wayahudi walijitenga sana na watu wa Mataifa - hawakuingia kwa nyumba zao wala kukula nao. Mungu alikuwa ameamba Petro kwa ndoto kwamba hata watu wa Mataifa watakuwa watu wake. Hili jambo lilikuwa ngumu kwa Petro kuelewa.

Petro alipokuja kwa nyumba ya Kornelio, alikumbuka chenye Mungu alikuwa amemwambia. Petro aliingia kwa nyumba ya Kornelio, alimkuta na familia yake na marafiki. Wote walikuwa wamekuja kumsikiliza Petro. Petro aliwambia kuhusu Yesu. Aliwambia kwamba Yesu hakutenda dhambi. Yesu alitoa uhai wake usio na mawaa msalabani. Mungu alimfufua kutoka kwa wafu. Petro alipokuwa bado anazungumza na Kornelio na familia yake, wote walipata Roho Mtakatifu. Petro alishangaa kuona Mungu amewapa watu wa Mataifa Roho Mtakatifu. Hii ilionyesha Petro kwamba Mungu anaokoa Mataifa pamoja na Wayahudi kupitia kwa Yesu.

Petro alibatiza Kornelio na familia yake. Walikuwa watu wa Mataifa wa kwanza kuwa Wakristo. Kupitia kwa ubatizo katika Yesu Kristo, watu wote wanakuwa watu wa Mungu. Watu wote wanaweza kuwa na tumaini la wokovu.